

USHIRIKA



Ulikuwa ujumbe wa kuchangamsha aliotupa Ndugu Pearry Green wakati huo kutoka kwa Neno la Mungu. Ni kweli jinsi gani ya kwamba “Tunamwekea Mungu mpaka na kumpa Mungu muda; naye ni wa Milele, hatuwezi kufanya hivyo.” Kwa hivyo usiku wa leo tunakabili jambo lingine, ushirika.

² Kwa miaka mitatu nilingoja kanisa lianzishwe Tucson, na ndilo hili. Naam, nasi—nasi tuko hapa. Kwa hivyo tunamshukuru Bwana, ametufanya tungoje hata wakati huu tunapoweza kulithamini.

³ Basi, kuna jambo moja ningetaka kusema kabla tu hatujaanza ushirika, nalo ni hili, ya kwamba tumeona ya kutosha katika siku tunazoishi, hata inatupasa kujitolea (kabisa) kwa Mungu. I—inatupasa kumtumikia Mungu kweli kweli. Naamini ametubariki sisi kwa jibu moja kwa moja la Maandiko. Kama Ndugu Perry alivyonena muda mchache uliopita, ya kwamba tu—tuko—tuko katika wakati huo. Sisi si vipofu, tu—tu—tunaona ya kwamba tuko hapa, tu—tumewasili.

⁴ Pia tunaweza kutazama pande zote na kuona jinsi akili za mwanadamu zinavyowatoka watu. Ya kwamba, ha—hatuwezi kukawia zaidi sana, tungekuwa katika kituo cha wenda wazimu, kabisa, ulimwengu mzima ungekuwa hivyo. Mwaona? Kwa hivyo tu—tuko katika wakati wa mwisho.

⁵ Naam, kama Ndugu Perry alivyomalizia pale, kwa kuwa mambo haya ni kweli, angalieni kama ni kweli, hayo si hadithi. Si mambo tu tunayowazia, ni mambo ambayo tumepewa sisi moja kwa moja na Neno la Mungu, na kudhihirishwa waziwazi mbele zetu, hata tunajua tuko hapa. Ha—hatujui kwa muda gani sasa, kwa maana tunarudi kwenye zamu, mwaona, ni wakati gani. Bali sisi... tunajua—tuko hapa, tumefikia wakati huo. Kama ni wakati wa Mungu, ningewazia...

⁶ Mtu mmoja alitoa maelezo madogo yaliyosema ya kwamba kama Mungu angalimvumilia kulingana...kama angaligawanya wakati, mi—miaka elfu moja ni siku moja tu. Kama mtu akiishi miaka sabini, ingekuwa dakika chache kwa majira ya Mungu. Unaona? Vema, inasemekana kuwa miaka arobaini, hiyo hata haingemaanisha wakati, hata, wa kupepesa jicho Lake. Waona? Oneni, ni upesi hivyo, jambo lote, kama—kama ingalipangiwa muda; ambapo, Yeye hana muda wo wote. Kwa hivyo Yeye ni wa Milele.

⁷ Naamini ilikuwa Sara kule nyuma, ama maskini Joseph usiku uliopita, akaniambia mimi pamoja na Ndugu Pearry, kasema, “Baba, ni wapi, Mungu alijitokeza lini jukwaani? Yeye

alitoka wapi?” Unuona? “Hapana budi alikuwa na mwanzo, sivyo? Je, Yeye alikuwa na mwanzo?”

⁸ Nikasema, “Sivyo. Kilicho na mwanzo kina mwisho, bali kisicho na mwanzo hakina mwisho.” Bali, bila shaka, yeye ana umri wa miaka kumi, hilo lilikuwa gu—gumu sana kwake. Waona? Naye angepokeaje hilo, kujua kwamba kitu fulani hakina mwanzo kamwe? Siye tu, bali mimi pia. Mnaona? Sisi sote, mwaona, ni—ni jambo kubwa mno kwangu, jinsi ilivyoanza.

⁹ Basi tunakaribia kuadhimisha jambo fulani hapa ambalo ni takatifu sana.

¹⁰ Naliitwa siku chache zilizopita, kwa mwungwana mmoja Mkristo ambaye—ambaye hakuwa amekuwa na hili kamwe, naye alifahamu ya kwamba tunashiriki Meza ya Bwana hasa. Wao hushiriki wanayoitwa “ushirika wa rohoni.” Ambao, tukinena kuhusu *ushirika*, ningesema ni sawa, maana *kushiriki maneno* ni “kuongea na,” mwaona. Naye huyo Ndugu akanipa Andiko hili, kasema, “Ndugu Branham, je, hufikiri sasa . . .”

¹¹ Sasa, sababu ya kusema hili . . . Ni vema, Ndugu Pearry? [Ndugu Pearry Green anajibu, “Bila shaka.”—Mh.] Mnaona, hiyo ndiyo sababu ya kusema hili, kusudi mfahamu mnayofanya. Wewe hau . . . kama ukiingilia jambo lo lote kijinga, hujui ni wapi, kile unachotenda. Hauwezi hata kuwa na ujasiri, kama haujui unachofanya. Bali inakupasa kufahamu unayofanya na sababu ya kufanya hayo.

¹² Yeye alisema, “Basi, tukishiriki Neno la Mungu, si huyo ni Mungu tunayemshiriki?”

¹³ Nikasema, “Kweli hasa, bwana, ni kweli. Bali tunasoma hapa ya kwamba wao bila shaka . . . Paulo alifundisha kushiriki Meza halisi ya Bwana. Fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu, akasema Yesu. Maana kila mwulapo huu kwa ukumbusho Wangu, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.” Mnaona? Basi, inatupasa kushiriki.

¹⁴ Tunafahamu ya kwamba Mtakatifu Paulo, ndiye aliyeiagiza Kanisani, akiwa nabii wa Agano Jipya. Petro, Yakobo, Yohana, wote hao, waliandika (naam, Mathayo, Marko, Luka) yale Yesu aliyotenda, kama waandishi. Bali Paulo aliweka mambo katika utaratibu, yeye alikuwa—yeye alikuwa nabii wa Agano Jipya. Kama vile tu Musa alivyoenda jangwani akapokee upako ili kuandika vile—vile Vitabu vitano vya—vya . . . Vile Vitabu vya kwanza vitano vya Bibia, vema, Paulo pia alienda jangwani na kupokea upako kutoka kwa Mungu, ili kuweka utaratibu katika Kanisa la Agano Jipya na kulifaninisha na la Kale.

¹⁵ Chini pale walikuwa na mwana-kondoo wa sadaka, ambaye Israeli walimhifadhi kwa ajili ya ukumbusho. Alitumiwa hasa mara moja walipokuwa wanatoka Misri. Na ndipo wakaendelea

kufanya hivyo kwa ukumbusho wakati huo wote. Vema, “ikiwa torati ni kivuli cha mambo yajayo,” unaona.

¹⁶ Sasa, ninaamini ya kwamba *ushirika* (tunachoita “ushirika,” sasa) niku . . . ni “meza ya Bwana.”

¹⁷ Naam, tuna tu maagizo matatu ya Kiungu tuliyoachiwa: mojawapo ni—ni ushirika; kutawadhana miguu; ubatizo wa maji. Hayo ndiyo tu mambo matatu. Huo ndio ukamilifu, wa utatu, mnaona. Na hayo ndiyo tu maagizo matatu tuliyo nayo. Twatambua ya kuwa hilo ndilo jambo lililotolewa na Mt. Paulo katika Agano Jipya.

¹⁸ Sasa, kama tungenesema “ushirika unapaswa uwe tu kupokea Neno,” siamini ye yote ana haki ya kushiriki meza ya Bwana mpaka kwanza amelipokea Ne—Neno la Bwana moyoni mwake. Mwaona? Kwa sababu nitaenda . . . Nitawasomea kitu fulani kwa dakika chache nanyi mtaona. Sasa, tazameni. Basi, mbona basi sisi tunge . . . sisi tunge . . .

¹⁹ Kwa msingi ule ule tungewahesabia haki Jeshi la Wokovu. Wao hawaamini namna yo yote ya ubatizo wa maji, kasema, “Hatuuhitaji.” Basi, iwapo hatuhitaji ubatizo wa maji, mbona tunabatizwa? Kasema, “Maji hayawezi kukuokoa, Damu ndiyo inayokuokoa.”

²⁰ Nakubaliana na hayo. Hiyo—hiyo ni kweli, Damu ndiyo inayokuokoa, si maji. Bali hatuna budi kuchukua maji kama onyesho la nje ya kwamba kazi fulani ya ndani, ambayo ni ya neema, imekwisha kufanyika. Mnaona? Yatupasa kufanya vivyo hivyo kwa ushirika!

²¹ Tunapompokea Bwana, Dhabihu yetu, ndani yetu, kama tendo la kuzaliwa Kiroho ndani yetu, na Mwili Wake, tukaishi kwa Neno Lake, inatupasa kuonyesha hayo kwa mfano kwa maana ni amri. “Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu.”

²² Paulo alisema, “Nimepokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, ‘ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, akaumega na kuwapa wanafunzi, na—na kusema, “Twaeni mle, fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu.” Kwa maana kila mwulapo mkate huu, mwaitangaza mauti Yake hata ajapo.” Sasa twaona ya kwamba, katika hayo, walikuwa na watu waliokuja na . . .

²³ Huyu ndugu mpendwa, ndugu mwema sana, alikuja na kusema, “Sija—sijaishiriki kamwe, Ndugu Branham, sifahamu ni nini.” Kasema, “Nimefundishwa upande huo mwingine.”

²⁴ Nikasema, “Lakini kumbuka, tutakubali ya kwamba Paulo aliweka katika utaratibu katika Kanisa la Kikristo la mwanzoni. Walienda kutoka kanisa . . . nyumba kwa nyumba, wakiumega mkate kwa moyo mmoja, na kadhalika. “Basi,” nikasema, “yeye aliweka Kanisani. Galatia 1:8, yeye alisema, ‘Kama malaika kutoka mbinguni akija na kusema neno lingine,

na alaaniwe,’ mwaona, oneni, mtu yule yule aliyewafanya wabatizwe tena kutoka ubatizo wa Yohana, wakabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.”

²⁵ Mwaona, kuna mambo matatu ambayo hatuna budi—mambo matatu yatupasayo kutenda kama mifano: meza ya Bwana, kutawadhana miguu, ubatizo wa maji. Mnaona? Kuna . . .

²⁶ Mnasema, “Vema, wale . . .” Naam, Jeshi la Wokovu huchukua kutoka kwa jambo kwamba, “Yule mwizi mautini, alipokufa hakuwa amebatizwa bado, Yesu alisema huyu atakuwa Mbinguni.” Hiyo ni kweli hasa. Ndivyo hasa. Bali, mwaona, a—a—alimtambua Yesu papo hapo tu katika saa ya kufa. Mwaona? Hiyo ndiyo tu—hiyo ndiyo tu nafasi aliyokuwa nayo. Yeye—yeye alikuwa mwizi, alikuwa mbali, alikuwa nje. Naye, mara alipoiona hiyo Nuru, akaitambua, “Bwana, nikumbuke!” Naye Yesu . . . Hiyo ilikuwa kweli.

²⁷ Bali kwako na kwangu tunaojua inatupasa kubatizwa, na kukataa kufanya hivyo, basi hiyo itakuwa kati yako na Mungu. Jambo lile lile katika ushirika!

²⁸ Sasa, tunapoupokea huu ushirika, si kusema tu, “Naja huku nikale mkate, nami nitaamini mimi ni Mkristo.” Bali, ukitazama, Biblia ilisema, “Yeye alaye na kunywa *isivyostahili* atakuwa amejipatia hatia ya Damu na Mwili wa Bwana.” Unaona? Inakupasa kuishi maisha ambayo—ambayo . . . mbele za watu, ambayo . . . na mbele za Mungu na watu, yanayoonyesha ya kwamba wewe—ya kwamba u mwaminifu.

²⁹ Naam, hebuni kwa muda mchache zaidi. Sasa, katika Agano la Kale wakati dhabihu ilipofanywa a—amri au agizo. Vivyo hivyo ubatizo wa maji ni agizo; kutawadhana miguu ni agizo pia; meza ya Bwana ni agizo pia. “Heri yule atendaye maagizo Yake yote, anayetii torati Zake zote, amri Zake zote, apate haki ya kuingia katika ule Mti wa Uzima.”

³⁰ Sasa, tazama hili sasa, ya kwamba mara ya kwanza, wakati ilikuwa kwanza agizo la Mungu kuleta dhabihu kanisani, na hekaluni na madhabahuni, na kutoa dhabihu yako, na—na kwa ajili ya dhambi zako, dhabihu ya mwana-kondoo. Vema, naweza tu kuwaza ndugu wa Kiyahudi akija barabarani, akijua ya kwamba yeye alikuwa mwenye hatia, naye aenda madhabahuni; ama analeta ng’ombe wake mnono ama fahali, au cho chote alichokuwa nacho, ama kondoo mume, mwana-kondoo, cho chote kile. Alikuwa amekuja nayo barabarani mwaminifu amwezavyo kuja, akaenda pale, akitii agizo la Mungu kwa uaminifu kabisa.

³¹ Kisha akaweka mikono yake juu yake, akikiri dhambi zake, naye kuhani akiweka hii (dhambi zake) juu ya huyo mwana-kondoo, kisha shingo ya huyo mwana-kondoo ilikakatwa, na—basi akafa kwa ajili yake. Alipokuwa amelala pale, huyo maskini mwana-kondoo akipigapiga mateke na kutokwa na

damu, huku mikono yake imejaa damu, nayo ikimiminikia mwili mzima, (huku huyo maskini mwana kondoo akilia, akifa) yeye angetambua alikuwa ametenda dhambi na kitu fulani kilipaswa kufa kwa ajili yake. Kwa hivyo, yeye alikuwa akitoa mauti ya mwana-kondoo huyu kwa ajili ya kifo chake. Waona, huyo mwana-kondoo alikufa mahali pake. Basi mtu huyu alifanya hayo kwa uaminifu, kwa unyenyekevu wa moyo wake.

³² Hatimaye, ikarudiwa na kurudiwa tena, ikaendelea kutendwa hata mwishowe ikawa mapokeo. Amri ya Mungu ikawa mapokeo kwa watu. Kisha ndiye huyu anashuka, “Vema, hebu tuone, huyu ni *fulani*—*wa-fulani* leo, labda yanipasa kwenda kule. Naam, yanipasa kutoa fa—fahali.” Akashuka. “Vema, Bwana, ndiye huyu fahali wangu.” Mnaona, hamna uaminifu kwake, hamna ufahamu kwake.

³³ Naam, hatutaki kupokea ushirika hivyo. Ni jambo lilo hilo tunapokuja kwenye meza ya Bwana.

³⁴ Isaya 35...la, samahani, Isaya 60...Hebu nirudishe hilo. Na—na—naamini ni Isaya 28, ndipo tunapopata hili. Nina hakika hiyo ndiyo sura yenyewe. Yeye alisema, “Amri ni lazima iwe juu ya amri; na kanuni juu ya kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa. Na hii ndiyo Raha.”

³⁵ Yeye alisema, “Meza zote za Bwana zimejaa matapiko. Nitamfundisha nani maarifa? Nitamfahamisha nani?” Mwaona? Naamini hilo ndilo Andiko halisi, Isaya 28. “Ni nani ninayeweza kumfahamisha Maarifa?” Mwaona, “zile meza.”

³⁶ Basi, tunaona ya kwamba leo jambo hili kuu tunalokaribia kufanya usiku huu, kwa ukumbusho wa mauti Yake na Mwili Wake tunaoamini tunaula kila siku, ama, tumekwisha kuula sasa hivi kama vile ndugu yetu alivyotuhubiria. Tukichukua Neno la Mungu tunaliamini kwa moyo wetu wote. Tunaliona likidhihirishwa, tunaliona likitolewa kwetu; tunaliona limethiirishwa; tualisikia maishani mwetu. Na inatupasa kulijia hili tukijua waziwazi yale tunayofanya, si eti kwa sababu ni agizo.

³⁷ Unahudhuria kanisa fulani, na mara nyingi wanatoa mkate mwembamba mgumu wenye chachu ama baadhi ya ki—kitu, wakauvunja-vunja, mkate mwembamba au—au kitu fulani, na—na kuuvunja-vunja; na watu wanaovuta sigara, wanaokunywa pombe, na kadhalika, kwa maana wao ni wafuasi wa kanisa hilo wanakuja na kupokea meza ya Bwana. Vema, huo ni uchafu mbele za Mungu!

³⁸ Hata zile sadaka, kasema, “Sikukuu zenu na sadaka zenu zimekuwa uvundo puani Mwangu.” Walakini aliwaagiza watoe hizo sadaka. Bali walivyozitendea, zikawa uvundo, ikanukia puani Mwake (mapua Yake), sadaka ile ile aliyoagiza.

³⁹ Hivyo ndivyo tunavyolipokea Neno la Mungu, Wakristo wengi sana siku hizi (wanavyodhaniwa) hufanya hivyo. Tunasimama humu na kufundisha Neno hili, na kusema, “Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele,” na kufundisha mambo ambayo Yeye alituahidi sisi ya kwamba atatimiza na kusema, “Loo, vema, hayo yalikuwa ya kitu kingine,” ibada zetu za Sodoma zimekuwa uvundo puani Mwake. Yeye hatazipokea, kwa vyo vyote vile. Hiyo ndiyo sababu yake, kwa tabia zetu za mapokeo!

⁴⁰ Hupokei meza ya Bwana kwa mapokeo. Unaipokea kwa sababu ni upendo wa Mungu moyoni mwako, kutii amri za Mungu. Unaona, unaipokea kwa sababu hiyo.

⁴¹ Kwa hivyo usipoipokea kwa unyenyekevu, ni mapokeo tu, “Vema kanisa letu hupokea ushirika mara moja kila Jumapili, mara moja kwa mwezi, ama mara mbili kwa mwaka,” nawe waenda huko na kusema, “Vema, ni zamu yangu,” kisha—kisha ukapokea ushirika, naam, ni uvundo kwa Mungu! Unaona, hayo ni mapokea tu.

⁴² Hata kama ilivyo kwa kila kitu, hu—huna budi kuwa mwaminifu. Mungu anataka kilindi cha moyo wako. Kumbuka Mungu yule yule aliyekuleta hapa ulimwenguni ndiye unayemtumikia. Unaona?

⁴³ Unafanya hili kwa sababu Yeye alisema hivyo, kwa sababu ni agizo Lake. Basi tunataka tuje kwa uaminifu sana, tukijua kwamba kwa neema ya Mungu tumeokolewa. Nasi—nasi tunampenda na tunasikia Uwepo Wake, na—na tunaona ukibadilisha maisha yetu. U—utu wetu wote umebadilishwa. Si—si—sisi tu watu tofauti. Hatuishi kama tulivyokuwa tukiishi, hatuwazi kama tulivyokuwa tukiwaza.

⁴⁴ Kama katika Kitabu hapa, na mahali pale tulipokuwa tukinena habari za—za vile Vitabu viwili kuwa Kimoja, kile Kitabu cha Uzima. Kitabu cha kwanza cha Uzima kikija, ilikuwa wakati ulipozaliwa, huko kulikuwa kuzaliwa kwako kwa kawaida. Unaona? Bali wakati mmoja, kule nyuma kabisa, kulikuweco chembe ndogo ya Uzima kama nilivyowaeleza baadhi ya dada wadogo kule nyumbani adhuhuri ya leo. Unaona, kuna chembe ndogo ya Uzima iliyoko mle ambayo ungeshangaa, “Je, ilitoka wapi? Nini—nini—mambo haya ya ajabu?”

⁴⁵ Nilikuwa nikisema hili, nikinena kwa niaba yangu mwenyewe, kama ungalisema, “William Branham, vema, miaka arobaini iliyopita, yule William Branham, yuyu huyu usiku huu.” Na mtu fulani nyuma kule angesema, “. . .? . . .yeye alikuwa mlaghai kweli kweli.” Waona? Kwa sababu nilizaliwa na Charles na Ella Branham. Katika asili yao nilikuwa mwenye dhambi, nikaja ulimwenguni, mwongo, na tabia zote za ulimwengu zilikaa ndani yangu. Bali humo ndani, pia, kulikuwa na Asili

nyingine, waona, iliyochaguliwa tangu awali, iliyowekwa mle na Mungu. Katika mwili uu huu, waona, asili mbili mle ndani.

⁴⁶ Vema, nilishughulikia moja tu. Na ilipokua, nilipasa sauti kama mtoto mchanga. “Dad—da.” Punde si punde, nikawa mwongo, nikawa cho chote ambacho ni chenye dhambi, kwa sababu nilikuzwa hivyo. Basi ndani mle mlikuwapo chembe ndogo ya Uzima wakati huo wote.

⁴⁷ Nilikuwa nikikumbuka, kama mvulana mdogo... (natumainia siwakawishi sana. Bali nikijua...) Nikiketi kule nje kwenye... u—ukingoni mwa ghuba ndogo, nami ningeketi mle na kutazama pande zote usiku. Baba na Mama, wamekwisha kwenda rahani mwao. Na siku hizo wao walikuwa wenye dhambi, hamkuwepo Ukristo nyumbani mwetu hata kidogo. Naam, jamani, kunywa pombe, karamu, na kufanya yasiyofaa; ilinichukiza, nami ningechukua taa yangu pamoja na mbwa wangu na kuenda msituni, kukaa humo usiku kucha. Katika majira ya baridi ningaliwinda hata karamu zilipokwisha, labda kwenye mapambazuko. Narudi nyumbani, la, hazijakwisha, ningejilaza juu ya kibanda na kulala usingizi, nikingojea mapambazuko.

⁴⁸ Ndipo ningewazia habari za majira, wakati huo nikiwa kule nje katika majira ya kiangazi, nichukue vijiti vyangu na kuvifanya viziue upepo, kama ingalinyesha; nilale hapo huku vijiti vimechomoza majini, nikivua samaki; maskini mbwa wangu ameketi pale. Ningesema, “Tazama hapa. Wajua, katika majira ya baridi yaliyopita nilipiga kambi papa hapa usiku mmoja, nikawasha moto papa hapa nilipokuwa nikimngojea maskini mbwa wangu afukuze mnyama, nami niliwasha moto hapa. Ardhi iligandamana kwa baridi kina cha inchi tano. Basi, maskini ua wee, ulitoka wapi? U—u—ulitoka wapi? Ni nani aliyekuja hapa akakupanda? Nao walikutoa kwenye kibanda kipi cha kuoteshea maua? Au—au je, ulitoka wapi?” Waona? Hilo ua ndogo, ningesema “Naam, ardhi ilikuwa imegandamana, na kadhalika, nami nikawasha moto juu hapa. Mbali na sehemu zilizogandamana, kulikuweko na hali ya joto humu juu ya gogo kubwa la kale nililolichoma moto. Hata hivyo ndiwe huyu, u hai. Je, ulitoka wapi?”

⁴⁹ Ilikuwa nini? Kulikuwepo William Branham mwingine. Mwaona? Doa ndogo la Uzima wa Milele mle, kutoka katika che—che—chembechembe hai za Mungu, Neno la Mungu lililowekwa mle ndani. Kila mmoja wenu anaweza kuwazia mambo kama hayo. Mwaona, lilikuwa likitenda kazi.

⁵⁰ Kisha nilitazama mitini na kuwaza, “Jani, nilikuona ukipukutika mwaka uliopita, nawe umerudi hapa tena? Ulitoka wapi? Nini kilikuleta hapa?” Waona, ilikuwa huo Uzima wa Milele ukitenda kazi katika mwili huo.

⁵¹ Basi, ndipo siku moja nilipokuwa nikitembea, hiyo Sauti ikanena, “Usivute sigara kamwe, usinywe pombe, na kadhalika.” Na hao vijana wote na kadhalika wakakomaa. Waona, kulikuwa na kitu kilichokuwa kikitenda kazi.

⁵² Walakini mara nilitazama juu, na kusema, “Mimi si mwana Charles na Ella Branham. Kuna Kitu kinachoniita.” Kama tai wangu, “Mimi si kuku. Kuna Kitu fulani kumaskini wale ng’ambo, mahali fulani. Ee Yehova uliye Mkuu, hata uwe nani, nifungulie! Nataka kuja nyumbani. Mna Kitu fulani ndani yangu, kinachoita.”

⁵³ Kisha nikazaliwa mara ya pili. Huo Uzima mdogo ulikuwa mle, uhai wa maji ukamwagiliwa Humo, kisha ukaanza kukua. Naam, hayo maisha ya kale yalisamehewa, yakawekwa kwenye bahari ya usahaulifu wa Mungu, yasije yakakumbukwa dhidi yangu tena. Mwaona? Sasa tumekwisha kuhesabiwa haki (kama kwamba hatukutenda dhambi kamwe) Mbele za Mungu.

⁵⁴ Basi tunapokuja kwenye meza ya Bwana, inatupasa kuja kwa unyenyekevu, upendo na heshima, ya “Tazama mahali tungalikuwa isingalikuwa kwa ajili Yake.” Mwaona? Tazama ambapo ingalikuwa. . .

⁵⁵ Kwa hivyo, Paulo, nafikiri, katika kusema hili, “Kwa hiyo, mkutanikapo mpate kula, mngoJane.” Hiyo ni kusema, kwa maneno mengine, ngoja tu kwa dakika chache, omba, jichunguze. Na iwapo unajua mna ndugu fulani humu, aliye jaribu kufanya jambo baya, ama cho chote kile, basi mwombe, pia. Waona? Waona, “mngoJane,” ngojeni kwa kitambo kidogo tu, ombeni. Iwapo mna neno ninyi kwa ninyi ama cho chote kile, msi—msifanye hivyo—msifanye hivyo, nendeni mkasuluhishe hayo kwanza. Mwaona? Nendeni mkanyoshe hilo kwanza, kwa sababu wanataka kuja hapa wakiwa wasafi iwezekanavyo, na tunayowaziana sisi kwa sisi na kwa Mungu, na mmoja kwa mwingine, ndiposa tunakuja kushiriki katika meza ya Bwana. Mwaona?

⁵⁶ Nasi hufanya hivi kwa maana tunamtolea Yeye shukrani, na sisi kwa sisi. Tukila mkate sisi kwa sisi, tukinywa divai sisi kwa sisi, kama Damu Yake na Mwili Wake.

⁵⁷ “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.” Mnaona? Mnaona, hivyo ndivyo Biblia ilisema. Msipofanya hivyo, hamna Uzima. Mnaona? Hapo basi wewe, kwa kadiri, unaonyesha unaona haya kujitambulisha mwenyewe kama Mkristo, kwa sababu ya maisha unayoishi. Ndiposa hili ndilo shindano la kuamua. Tena usipofanya hivyo, hauna Uzima. Kama ukifanya hivyo isivyostahili, una hatia ya mwili wa Bwana.

⁵⁸ Jambo lile lile katika ubatizo wa maji. Kama tukisema, “Tunamwamini Yesu Kristo, Yeye alituokoa kutoka dhambini, nasi tunabatizwa katika Jina la Yesu Kristo,” naam, tuna—

tunamletea Yeye aibu, tunafanya mambo mabaya na i—itatulazimu kuyajutia. Na jambo lingine, ni kwamba tunapofanya hivyo, tunajaribu kukiri jambo moja na kutenda lingine.

⁵⁹ Hiyo ndiyo shida yetu leo. Ninavyofikiri... Mimi ninasema “sisi,” mimi, na kanisa la Bwana ambalo Mungu ameniruhusu kuzungumzia katika majira haya ya mwisho, ambapo tunaamini tuko katika wakati wa kumalizia. Tunaamini ya kwamba Mungu ametupa Ujumbe. Umeamriwa na Mungu, Umethibitishwa na Mungu, Umeonyeshwa na Mungu. Sasa inatupasa kumjia Yeye kwa unyenyekevu na kwa upendo, na kwa—kwa weupe wa moyo na nia na nafsi.

⁶⁰ Mnajua, saa itakuja hivi karibuni ambapo—ambapo mumu humu miongoni mwetu kuta... Roho Mtakatifu atanena kama alivyofanya katika Anania na Safira. Mwaona, hiyo saa inakuja. Mwaona? Nasi tuna... Naam, kumbukeni hayo tu, mnaona, ya kwamba Mungu ataishi kati ya watu Wake. Hivyo ndivyo anavyotaka kufanya sasa.

⁶¹ Tungepokea Ujumbe tukisema... Kama nilikuwa kijana mwanamume na—na huku namtafuta mke, nami ningempata mke, nikasema, “Yeye ni mkamilifu kabisa. Yeye ni Mkristo. Yeye ni bibi. Yeye ni haya yote, nina matumaini.” Haijalishi nina matumaini jinsi gani, jinsi ninavyofikiri yeye ni mzuri, sina budi kunipokea, hana budi kunipokea; unaona, juu ya nadhiri hizi.

⁶² Vema, ni jambo lile lile tunaloona kuwa ni Ujumbe. Tunaona ni kweli. Tunaona Mungu akiuthibitisha kuwa kweli hasa. Ni kweli kabisa. Mwaka baada ya mwaka, mwaka baada ya mwaka, unazidi kuwa kweli, unaaendelea ukiwa kweli. Kila kitu usemacho, kinatimia jinsi hasa Yeye alivyosema. Naam, tunajua ni kweli, bali, unaona, usifanye hivyo, kutoka kwa msimamo wa kielimu. Ukifanya hivyo, una dini iliyokwisha kutumiwa. Waona? Hatutaki dini iliyokwisha kutumiwa, kitu ambacho mtu mwingine amekwisha kujaribu nasi tunaishi kwake—kwa ushuhuda wao.

⁶³ Naamini ni Yesu aliyemwambia Pilato, jambo fulani, neno nililokuwa nikiwazia, Naye alisema hapo muda mchache tu uliopita, “Ni nani aliyekwambia hayo?” Ama, “Je, yalifunuliwa kwako? Ulijuaje mambo haya?” Kwa maneno mengine. Sijui ni neno gani sasa, ni muda mrefu tangu nilipolisoma, bali, “Ulijuaje—ulionaje yale... Je... Ni nani aliyekufunulia hili?” Juu ya Yeye kuwa Mwana wa Mungu. “Ni nani aliyekufunulia? Je, mtu fulani alikwambia hayo? Ama,” kama Yesu alivyosema, “ni Baba Yangu aliye Mbinguni aliyekufunulia?” Waona? Waona? “Ulijuaje hilo, kutoka kwa mwingine ama ni ufunuo mkamilifu kutoka kwa Mungu?”

⁶⁴ Je, ushirika huu ni jambo ninaloliendea tu, agizo fulani, kasema “Vema, wengine wao huupokea, nitafanya hivyo pia”? Ni

ufunuo ya kwamba mimi ni sehemu Yake nami ni sehemu yenu, nami nawapenda na ninampenda Yeye, pia, nasi tunaupokea huu pamoja kama mfano wa upendo wetu kwa Mungu, na upendo wetu pamoja na ushirika wetu sisi kwa sisi.

⁶⁵ Sasa nataka kusoma machache kutoka kwa Maandiko. Ndiposa nakisia...Ni wapi ninyi...Kwa njia yoyote Ndugu Pearry atakayo leo. Ningependa msome pamoja nami, iwapo mna Biblia zenu. I Wakorintho, su—sura ya 11, tukianzia mlango wa 23.

⁶⁶ Halafu pia, kwenye maskani yetu, daima tumeadhimisha hili na kutawadhana miguu, kila mara, kwa sababu yanaabatana pamoja. Naamini ndugu alitangaza “Jumatano usiku” kwa sababu ya umati na hamna ya...nafasi ya kutosha kuwaleta watu kwa ajili ya kutawadhana miguu, wao wataadhimisha—wataadhimisha hayo Jumatano usiku.

⁶⁷ Basi, kifungu cha 23 cha sura ya 11 ya 1 Wakorintho, msikizeni Paulo sasa. Sasa kumbukeni na msisahau haya, Wagalatia 1:8, “Ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote,” (isipokuwa Injili hii aliyokuwa amehubiri) “na alaaniwe.” Mwaona?

Kwa maana mimi nilipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kwamba Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate.

Naye akiisha kushukuru akaumega, . . .kasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

⁶⁸ Naam, hebu nikome papa hapa, niseme. Lakini kula mwili wa Bwana Yesu Kristo katika ushirika huu hakumaanishi ya kwamba ushirika ni mwili halisi wa Kristo. Hiyo ni Katoliki. Siamini ya kwamba hiyo ni kweli. Naamini ni agizo tu ambalo Bwana alituagiza, mwaona, si mwili halisi. Ni...Naam, bila shaka ni kipande cha mkate usiotiwa chachu. Ni agizo tu.

⁶⁹ Wala siamini ya kwamba ubatizo wa Yesu Kristo (katika Jina la Yesu Kristo) katika maji hukusamehe dhambi zako. Siamini ya kwamba wewe...Naamini ungebatizwa siku nzima... Sasa, najua labda mna watu wanaoketi humu wanaotoka kwenye kanisa la Apostolic, namaanisha, ama kanisa la United Pentekoste, ambalo hufundisha hayo. Ila, mwaona, si—siamini ya kwamba ubatizo wa maji husamehe dhambi. Au, kama unafanya hivyo, basi Yesu alikufa bure. Ona? Naamini ya kwamba ni agizo tu la Mungu, waona, kuonyesha ya kwamba umekwisha kusamehewa. Bali kubatizwa kwa ajili ya kuzaliwa mara ya pili, la, si—si—siamini hilo. Siamini ya kwamba maji husamehe dhambi.

⁷⁰ Wala siamini ya kwamba huu mkate pamoja na divai vinawahusu kamwe, ni kuadhimisha tu agizo ambalo Mungu ametuagiza kufanya. Mwaona? Hiyo ni kweli. Naamini ubatizo

wa maji ni jambo lile lile. Naamini inatupasa kufanya hivyo, ya kwamba Yeye alifanya hayo yote kwa kielelezo chetu. Naye alifanya hili kwa kielelezo chetu. Alitawadhana miguu kwa kielelezo chetu.

⁷¹ Sasa, “Na vivi hivi,” kifungu cha 25:

Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.

Maana kila... (Kumbukeni sasa!)... Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. (Kwa muda gani? “Hata ajapo!” Mwaona? Mwaona?)

Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.

⁷² Hebu nikome kwa dakika tu. Kusudi la yeye kusema haya, mliona katika kifungu kingine hapa, sura nyingine, ya kwamba yeye alisema, “Nasikia mnapo—mnapokutanika pamoja mnakula, hata kulewa kwenye meza ya Bwana.” Wao walielewa vibaya, mwaona. Wao walikuwa walafi, mnaona. Kama tu watu wanavyofanya siku hizi, wanaishi tu maisha yo yote na kuupokea. Mwaona? Naye akasema, “Mna nyumba za kulia, mwaona. Bali hili ni agizo linalotupasa kutekeleza, mwaona.” Basi:

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.

Maana alaya na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana. (Mwaona?)

⁷³ Wewe ni nini? Wewe ni Mkristo, basi ishi mbele ya kila mtu kama Mkristo. Na ukiupokea huo na huishi kama Mkristo, wewe huupambanui mwili wa Bwana. Unaweka jiwe la kujikwaa mbele ya mtu mwingine, waona, wanapokuona ukijaribu kufanya hivyo na huishi vile unavyopaswa kuishi. Unaona, wewe huupambanui mwili wa Bwana. Sasa tazama vile... laana yake ni nini:

Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. (Tafsiri halisi ya neno hilo, Ndugu Peary, ni “wamekufa.” Unaona? Waona, “watu kadha wa kadha wamekufa.”)

Lakini kama—lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa. (Mwaona, kama tukijipambanua nafsi zetu hatutahukumiwa. Mnaona?)

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije inatupasa adhabu pamoja na dunia. (Mwaona, tusihesabiwe pamoja na ulimwengu)

Kwa hivyo, ndugu zangu, mkusanyikapo mpate kula, mngojeane. (Mwaona?)

Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nitayatengeneza nijapo. (Mwaona?)

⁷⁴ Sasa, kwa maneno mengine, msije tu kuupokea kama... Kama nilivyosema muda mchache uliopita, kuhusu Wayahudi, dhahihu zao, wao... Zilikuwa za ajabu, zilitolewa na Mungu, bali ilifikia mahali ambapo hawakuzitoa kwa uaminifu na unyenyekevu na katika taratibu, basi zikawa tu... zikawa u—uvundo puani Mwake.

⁷⁵ Basi ni jambo lile lile tunapokuja kupokea meza ya Bwana, kwamba inatupasa kuikaribia tukijua tunachotenda. Kama tu wakati unapoingia majini kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, unajua inachofanya, unalionyesha kanisa kile Mungu ameweka ndani yako, Kristo.

⁷⁶ Unapoupokea huu, inaonyesha kanisa ya kwamba “Naamini kila Neno la Mungu. Naamini ya kwamba Yeye ni Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni. Naamini kila Neno asemalo ni Kweli. Nami naishi kwalo vizuri nijuavyo, Mungu akiwa Hakimu wangu. Kwa hivyo, mbele za ndugu zangu, mbele za dada zangu... si—situkani, silaani, sitendi mambo haya, kwa sababu nampenda Bwana, na Bwana ajua na ananishuhudia. Kwa hivyo, mbele zenu, nachukua kipande hiki cha mwili Wake, nikijua ya kwamba hainipati adhabu pamoja na ulimwengu.” Waona, ndivyo ilivyo, basi ni baraka.

⁷⁷ Naam, kumbukeni, ningetoa shuhuda nyingi kuhusu haya, ambapo nimechukua hayo na kuyaeleza kwenye chumba cha wagojwa, na kuona wakiponywa.

⁷⁸ Kumbukeni, Waisraeli walipokula mfano wa huu, walisafiri kwa miaka arobaini jangwani na nguo zao hata hazikuchakaa, nao wakafika bila kuwa na hata mmoja mdhaifu—mmoja kati yao, wakiwa watu milioni mbili kama mfano wa huu. Vema basi, kitu halisi kitafanyaje? Kama mwili wa mnyama wa sadaka uliwafanyia wao hayo, je, Mwili wa Yesu Kristo, Imanueli, utatufanyiaje? Na tuwe wanyenyekevu tunapokuja. Na tuwe wanyenyekevu sana tuwezavyo, tunapokuja.



USHIRIKA SWA65-1212

(Communion)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Desemba 12, 1965, kwenye Maskani ya Tucson kule Tucson, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org